**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA**

**Kumb. Na. AB.03/117/01/70** **18/5/2022**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa kupitia shirika la ICAP anawatangazia wananchi wote nafasi za kazi kama ifuatavyo:

1) Data Officers nafasi 4.
2) Wauguzi (ART Nurses) nafasi 2
3) Maafisa Tabibu (clinician ) nafasi 1
4) Maabara nafasi 2
5) Clinical Trackers (Nurses/Clinician) 5

### 1. DATA OFFICERS – Nafasi 4

**SIFA ZA MWOMBAJI.**

1) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
2) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
3) Awe na Stashahada ya sayansi ya Kompyuta , maswala ya takwimu za afya, takwimu au teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) au fani inayohusiana nayo, kutoka chuo kinachotambulikana na Serikali.
4) Uzoefu wa angalau miaka miwili (2) wa kufanya kazi kama afisa takwimu katika afua za VVU/UKIMWI
5) Uzoefu wa angalau miaka miwili (2) wa kutumia ya CTC2 na DHIS2
6) Ujuzi wa uchambuzi na utatuzi wa matatizo
7) Uwezo wa kufanya kazi kwa usimamizi mdogo
8) Uwezo wa kudumisha usiri katika nyanja zote.

**MAJUKUMU (Data Officer)**

1. Kuingiza taarifa kwenye kanzi data ya CTC 2 na DHIS2.
2. Kufanya kazi za uchambuzi wa taarifa CTC na kuandaa ili kurahisisha tathimini
3. Kupanga mafaili ya wagonjwa ili kurahisisha upatikanaji
4. Kuhakikisha mafaili ya wagonjwa yameingizwa kwenye mfumo ndani ya siku moja baada ya mgonjwa kuonwa na daktari
5. Kutayarisha, kuhakikisha na kutuma taarifa za HTS, upimaji wa index, PITC, PMTC na TB/VVU kwa mujibu wa ratiba iliyokubaliwa kila wiki, mwezi , robo.

6. Kuchambua na kutia orodha za wagonjwa mara kwa mara kwa ajili ya ufuatiliaji ka vile LTFU, IPT na HVL
7. Kuwezesha uchanganuzi na tafsri rahisi ya data katika ngazi ya kituo ili kuhimiza matumizi ya data kwa kupanga na kufanya maamuzi katika ngazi ya kituo
8. Kufuatilia hifadhi data mbali mbali kwenye kituo na kuwasiliana kwa maneno na kwa maandishi na wasimamizi kuhusu changamoti za hifadhi data
9. Kuhakikisha hakuna utofauti wa takwimu kati ya hifadhidata na vyanzo vya data.
10. Kuhudhuria mikutano ya wafanyakazi wa data kwa nyakati maalum
11. Kuwasilisha kwa maneno na kwa maandishi mapendekezo ya maboresho ya mifumo ya kitakwimu
12. Kusimamia masuala yote yanayohusu takwimu kituoni
13. Kutekeleza majukumu mengine ya data kama ilivyokabidhiwa.

## 2. WAUGUZI DARAJA II (ART NURSES) Nafasi 2 TGTS A

1) Awe raia wa Tanzania
2) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
3) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
4) Angalau ngazi ya kidato cha nne ya elimu ya sekondari.
5) Lazima Uwe Muuguzi mwenye stashahada kutoka katika chuo kilichosajiliwa na kutabulika na serikali.
6) Awe amesajiliwa na baraza husika.
7) Ujuzi kwenye kompyuta utakuwa faida ya ziada. (Ms Word, Excel, na MS)
8) Angalau uzoefu wa mwaka mmoja(1) wa kufanya kazi katika programu ya VVU/UKIMWI katika CTC.
9) Anajua Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha

**Kazi na Majukumu:**

1) Kuhudumia wateja wote (WAVIU na Wasio WAVIU) wanaohudhuria CTC ili kuhakikisha huduma za kliniki zinatolewa kulingana na miongozo ya kitaifa ya matibabu ya VVU.
2) Kuhakikisha wateja wote wanaohudhuria kwenye kituo chako wanapewa ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa mujibu wa miongozo ya wizara ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee, na watoto.
3) Kuhakikisha wagonjwa/wateja wote wanaohudhuria kwenye kituo chako wanachunguzwa ili kubaini ustahiki wao wa kupima VVU na wale wote wanaostahiki wanapimwa.
4) Kuwezesha na kufanya upimaji wa viashiria kwa wenzi wa ngono wa WAVIU waliotambuliwa hivi karibuni au wanaohudhuria huduma za CTC kwenye kituo chako .
5) Kuhakikisha wateja wote wanaotambulika kuwa na VVU wanaunganishwa na huduma ya tiba na matunzo na waanze kutumia ART siku hiyo hiyo (Siku hiyo hiyo ya kuanza kwa ART)
6) Hakikisha watoto wanaohudhuria kituoni wanachunguzwa kama wanastahili kupima na wenye sifa wapatiwe huduma ya upimji.

7) Kuhakikisha kuwa watoto wote wenye majibu chanya wanaanza kutumia ART
8) Kuhakikisha ufuasi mzuri kwenye ART kwa watoto hivyo basi kufanikiwa kufubaza virusi
9) kuhakikisha uchunguzi wa TB kwa WAVIU wote waliopo kwenye kwenye ART, washukiwa wamegunduliwa na kutibiwa na wale wanaostahili kupata IPT wanaanzishwa na kukamilika kwa mafanikio.
10) Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini (hakikisha uwekaji kumbukumbu sahihi wa huduma zote zinazotolewa na ripoti zinatayarishwa na kuwasilishwa kulingana na mwongozo wa MOHCDGEC
11) Tekeleza shughuli za PMTCT katika kituo chako afya.
12) Kutekeleza majukumu mengine kama utakavyopangiwa na msimamizi wako

### 3. MATABIBU (CLINICAL OFFICERS) DARAJA LA II TGHS B

**Sifa za mwombaji:**

1) Awe na cheti cha kidato cha nne na kuendelea
2) Stashahada ya utabibu kutoka katika chuo kinachotambulika na lazima awe imesajiliwa
3) Awe na leseni inayomruuhusu kufanya kazi anayoiomba.
4) Uzoefu wa miaka 2 au zaidi wa kutoa huduma ya kimatibabu ya VVU/UKIMWI
5) Uwezo wa kutumia lugha ya kiswahili na kiingereza kwa ufasaha.

**Kazi na majukumu:**

1) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu
2) Kuhudumia wateja wanaohudhuria CTC na kuhakikisha huduma inatolewa kwa mujibu muongozo wa huduma za tiba na matunzo
3) kuhakikisha wateja wote wanaohudhuria OPD na idara nyingine wanapewa huduma ushauri nasaha na upimaji wa VVU.
4) kusimamia huduma za upimaji wa VVU (HTS) kwa Uchunguzi wa wateja wa OPD ili kutambua wateja wanaostahili kupima VVU na Utoaji wa huduma za kupima VVU kwa wagonjwa wote wanaostahili
5) Kusimamia upimaji wa wenza, watoto walio chini ya umri wa miaka 15 na marafiki rika wa wenye maambukizi ya VVU/IKIMWI.
6) Kuhakikisha wateja wote wanaotambulika kuwa na maambukizi wanaanzishiwa dawa siku hiyo hiyo au ndani ya siku saba(Same day ART iniciatition)
7) Kufanya uchunguzi wa magonjwa nyemelezi kama kifua kikuu na kutoa huduma za kinga ya kuzuia kifua kikuu kwa wagonjwa wote wenye sifa.
8) Kuratibu na kushiriki katika kliniki za watoto Jumamosi na vilabu vya vijana kama njia ya kuboresha ufuasi na ufubazaji wa virusi.
9) Kwa kushirikiana na msimamizi wa CTC kuhakikisha kuna ukusanyaji wa sampuli za wingi wa virusi vya UKIMWI na sampuli zinakusanywa kila siku na kurekodiwa ipasavyo.
10) Kuhakikisha wanawake walio na VVU wanachunguzwa Saratani ya Shingo ya Kizazi na wale wanaopatikana na dalili waanzishwe matibabu au wapewe rufaa kwa ajili ya matibabu.
11) Kuhakikisha huduma zote zinazotolewa zimejazwa katika rejista zilizopo kulingana na mwendelezo wa matunzo ya VVU

12) kuratibu utoaji wa huduma, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya huduma za matunzo na matibabu, shughuli za RCH/PMTCT, utambuzi wa watoto wachanga mapema (EID) na shughuli shirikishi za TB/VVU.
13) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti za kila siku, wiki, mwezi na robo mwaka kwa mamlaka husika.
14) Kutekeleza majukumu mengine kama atakavyopangiwa na msimamizi wako

### 4. MAABARA: (MTEKNOLOJIA ) DARAJA II – TGHTS B

**Sifa Za Muombaji**

1) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
2) Awe na leseni
3) Awe na (Diploma) ya Utabibu kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi na majukumu:**

1) Kupima sampuli zinazoletwa maabara
2) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara za ngazi za juu
3) Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, viaa, kemikali na hifadhi ya kemikali
4) Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi
5) Kufundisha watumishi walio chini yake
6) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusika na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### 5. MATABIBU (CLINICAL Trackers)

**Sifa za mwombaji:**

1) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
2) Awe muuguzi au tabibu ngazi ya stashahada kutoka katika chuo kinachotambulika na serikali
3) Awe amesajiliwa na baraza husika na kuwa na leseni.
4) Angalau uzoefu wa mwaka mmoja (1) wa kufanya kazi katika afua za UKIMWI.
5) Awe anajua kusoma na kuandika kiswahili na kiingereza kwa ufasaha.
6) Awe na Uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea na katika timu
7) Kuzingatia kanuni na maadili ya kazi.
8) Kutunza siri za wateja
9) Mafunzo ya Msingi ya Usimamizi wa VVU/UKIMWI,

**Kazi na Majukumu:**

1. Kutambua wagonjwa waliokosa ratiba ya yao ya kliniki kwa wakati na kuwafuatilia kwa simu
2. • Kuandaa na kushirikiana na watoa huduma wa ngazi ya jamii au wateja bingwa orodha ya wafuatiliaji ya wateja ambao hawakupatikana kupitia simu na wale ambao hawana simu.
3. • Kuweka matokeo yote ya ufuatiliaji kwenye rejista ya ufuatiliaji
4. • Kuwezesha kuingizwa kwa matokeo ya ufuatiliaji katika kadi ya CTC 2 na database kwa kushirikiana na Afisa takwimu wa kituo.
5. • Kufanya ukaguzi wa kila wiki na kuhakikisha kuwa matokeo yote ya ufuatiliaji yanaingizwa kwenye rejista ya ufatiliaji na kuingizwa kwenye database ya CTC 2
6. • Kuhakikisha wateja waliokosa kupata huduma wanafuatiliwa kwa wakati na wanarejeshwa kwenye huduma kila mwezi
7. • Kufanya kazi na msimamizi wa rufaa, mshauri na afisa takwimu ili kuthibitisha uhamisho wote katika kituo husika
8. • Kutoa elimu ya afya kuhusu umuhimu wa kufuata kliniki kwa mteja na familia
9. • Kusaidia ufuasi wa mgonjwa wa dawa na ratiba za kliniki
10. • Kurekodi na kuripoti huduma za ufuatiliaji kila siku, kila wiki, kila mwezi na robo mwaka
11. • Kutayarisha muhtasari wa ripoti kila wiki, kila mwezi na robo mwaka na uwasilishe kwa msimamizi wa kituo.
12. • Shiriki katika shughuli za QI ambazo zinalenga kuongeza uboreshaji wa huduma katika kituo.
13. • Kutoa mawazo au maoni ambayo yanaweza kuchangia mfumo bora wa ufuatiliaji wa mgonjwa.
14. • Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama utakavyoagizwa na msimamizi wa kituo.

Maombi yaambatishwe na vivuli vya vyeti vya elimu na taaluma, pamoja na vyeti vya kuzaliwa vya mwombaji, CV, pia namba ya simu.

Ajira hii ni ya mkataba wa mwaka mmoja.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30/5/2022 saa 3.30 (Tisa na nusu) mchana.

Maombi haya yatumwe kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa,
S.L.P. 44,
**BUCHOSA**

Shija L. Lyella,
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA